**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 18 Juni, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2024/2025.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

287. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kila msimu wa mvua unapotufikia, jamii yetu hugawanyika katika makundi mawili makuu. Wako wananchi wanaoifurahia neema hii kwa kupanda miti na kufanya mambo mengine ya kimaendeleo, lakini hali hiyo huwa tofauti kwa wakaazi wanaoishi katika Ziwa Maboga kutokana na maji kuwaingilia majumbani mwao na kulazimika kuziacha nyumba zao na

kuhama huku baadhi ya mali zao kuathirika.

(a) Je, kwa muda gani sasa Serikali yetu inalihamu jambo hili.

(b) Kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu sana na lina athiri jamii, ni ipi kauli ya Serikali katika kuiondoa changamoto hii sugu.

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

249. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Takwimu zikoje juu ya kupungua kwa matumizi ya mkaa kwenye ngazi mbali mbali za vijiji vyetu.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

280. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika Kifungu cha 139(c)(iii) cha Ilani ya CCM, Serikali ilielekezwa kuendelea kupunguza asilimia ya utegemezi wa bajeti ili usizidi kiwango cha tarakimu moja na hivyo kuwa na uhakika wa kuendeleza mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imefikia lengo hilo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

184. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na kuwa na sheria inayodhibiti uhalifu wa kimtandao ikiwa ni pamoja na makosa ya kuwakashifu viongozi wetu kupitia mitandao mbali mbali ya kijamii, suala hili limeendelea kuzoeleka katika jamii yetu siku hadi siku.

(a) Je, Wizara yako inawashughulikia vipi wanaotoa maneno ya kejeli na kashfa kwa viongozi wetu kupitia mitandao mbali mbali ya kijamii.

(b) Nini ipi kauli ya Serikali juu ya watu wa aina hii ambao tumeanza kuona kila siku wanachipukia.

265. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Siku za hivi karibuni Serikali zote mbili za SMT na SMZ zilitoa kauli juu ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, huku baadhi ya watu wakiwa tayari wameshalipwa fidia ya mali zao na walio wengi bado hawajalipwa, wakisubiri kwa kipindi kirefu kulipwa fidia zao.

Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha ujenzi huo usianze huku watu wengi wakiwa hawajalipwa fidia zao hadi leo hii.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

126. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na changamoto kubwa katika mfumo wetu wa elimu ya juu katika tathmini kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Taarifa zinaonesha kuwepo kwa kiwango kikubwa cha udanganyifu, hasa katika mitihani ya tafiti (Thesis and Dissertation) kwa wanafunzi wa Uzamili. Kuongezeka kwa matumizi ya akili mgando (Artificial Intelligence) kumeongeza zaidi tatizo hili.

(a) Je, kwa tathmini iliyofanywa, ni kesi ngapi za udanganyifu zinazohusiana na mitihani ya tafiti (Thesis and Dissertation) zimeripotiwa katika vyuo vyetu hapa Zanzibar.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi ili kuwa na mfumo bora wa kudhibiti udanganyifu huu, ambao ni hatari kwa mfumo wetu wa elimu.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

73. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tunaiopongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwashajihisha wananchi wake juu ya suala la kilimo, pamoja na kuwepo kwa uhaba wa matrekta unaozorotesha shughuli za ukulima. Aidha, kuna taarifa kuwa yapo matrekta 38 kwa Unguja na Pemba ambayo ni mazima na matrekta 14 ambayo yanahitaji matengenezo.

(a) Je, kuna ukweli gani wa suala hili.

(b) Je, Wizara yako inawaeleza nini wakulima wa Zanzibar juu ya suala hili.

285. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kilimo cha 'horticulture' ni kilimo kinachofanyika katika nchi nyingi na huziingizia nchi hizo fedha nyingi za kigeni. Pamoja na kuanza kufanyika kwa kilimo hicho hapa Zanzibar, bado kuna changamoto kubwa ya kupatikana miche iliyobora na iliyozalishwa kwa kutumia teknolojia kama vile 'tissue culture'.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa inawapata wawekezaji watakaowekeza katika uzalishaji wa miche bora kwa kutumia utaalamu kama huu wa 'tissue culture'.

(b) Je, kwa sasa ni miche ya aina gani iliyo katika kundi la 'horticulture' hutolewa na Serikali ili kuwawezesha wananchi kuwa na kilimo kilicho bora zaidi.

(c) Je, tathimini inaonesha ni kiwango gani cha mazao ya 'horticulture' huingizwa Zanzibar kwa matumizi ya kila siku.

**Wizara ya Afya:**

85. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika Kituo cha Afya cha Mwambe kuna kituo kilichojengwa awali kwa ajili ya mama na mtoto ambacho kabla ya kumalizika kwake, watu wa Wizara ya Afya Pemba walikipendekeza kifanywe Kituo cha Kuzalia Wajawazito, kutokana na uzazi unaoendelea kuongezeka siku hadi siku. Kituo hicho kilifanyiwa maboresho yote ya kukimaliza lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote ya ujenzi wake inayoendelea.

(a) Kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu hili.

(b) Je, ni lini kituo hicho kitamalizika kujengwa.

210. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni vipaumbele gani na fursa zipi zinazopatikana kwa wazee wastaafu ambao walilitumikia taifa letu, pale wanapofika kwenye vituo vya kutoa huduma za afya nchini.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

108. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kulikuwa na taarifa kwamba Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) linakabiliwa na deni kubwa kutoka kwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kushindwa kulilipa kwa muda mrefu. Hali hii ilizuwa wasiwasi kati ya watumiaji wa umeme, wakihofia kuwa TANESCO huenda wakalikatia umeme Shirika la Umeme Zanzibar hadi watakapomaliza kulipa deni hilo.

(a) Je, kwa sasa Shirika linadaiwa kiasi gani na TANESCO na ni upi mkakati wa Shirika hilo katika kulilipa deni hilo.

(b) Je, Serikali inachukua mikakati gani ili kupunguza limbikizo kubwa la madeni yanayotokana na umeme kwa Shirika letu.

(c) Je, ni upi mpango wa muda mrefu wa Serikali wa kuhakikisha kuwa Zanzibar inavyo vyanzo vyake vya uhakika vya umeme.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

271. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwepo na uhitaji wa walimu wa kufundisha Kiswahili katika nchi nyingi duniani na baadhi ya nchi zimeweka mikakati ya kitaifa na vyuo vikuu vingi kuanzisha kozi za lugha ya Kiswahili. Aidha, kwa upande wa Afrika, kumekuwa na uhitaji mkubwa kutokana na Kiswahili kutumika katika Umoja wa Afrika (AU).

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kuwaandaa vijana na hatimae kuwaunganisha katika fursa hizi.

(b) Je, mpaka sasa, ni wanufaika wangapi walioandaliwa ambao tayari wameshapata fursa hizo na wangapi wapo katika mchakato wa kuandaliwa.

(c) Je, ni yepi maoteo ya mahitaji ya walimu wa Kiswahili ambao Zanzibar inatarajiwa kutoa na kuwasambaza katika nchi nyengine za Afrika na duniani.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**18 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**